# Nyayo:

## Simama uonekane, kuwa wewe!

### ¿Sabías qué?

Después de que Daniel y sus tres amigos fueran llevados cautivos a Babilonia, el Rey cambió sus nombres. Él quería convertirlos en babilonios (pero no funcionó).

**Lee Daniel 1:6-7 para ver cuáles son sus nuevos nombres.**

### Utangulizi wa somo

Somo hili la shule ya Jumapili ni pana sana. Unaweza kutamani uligawe katika vipengele na ulitumie katika madarasa mawili au matatu ya shule ya Jumapili.Kusudi la somo ni kwamba watoto waelewe mguso ambao Danieli aliuweka katika maisha ya Mfalme Dario na watoto wafikirie kuhusu mguso wanaoweza kuuweka kwa wenzao.

Maswali yaliyoandikwa kwa wino mzito ni msingi katika somo hili. Hakikisha unachukua muda kuwasikiliza watoto na uyaitikie majibu yao. Hakuna majibu yaliyokosewa. Watoto watumie mawazo yao na hali yao ya kiroho kuelewa Mungu anasema nini kwao. Sisi ni wawezeshaji tu.

***Kifungu cha Kukariri: Daniel 6:26-27***

***'....maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho. Yeye huponya na kuokoa, hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, ndiye aliyemponya Danieli na nguvu za simba.'***

### Utangulizi juu ya kiini - Nyayo za miguu:

***Nyayo za miguu***

***Maelezo ya nyayo za miguu***
*1: sura ya mguu juu ya udongo*

***Waulize watoto na usikilize majibu yao.***
***Umewahi kuona nyazo zako kwenye mchanga?***

*Unapokanyaga, unaacha alama ambayo inaweza kudumu mda mrefu baada ya wewe kuondoka.*
*Nyazo za miguu ni alama au sura iliyoachwa nyuma na mtu aliyekuwa anatembea au anakimbia.*

***Waambie watoto waitizame miguu yao, umbo lake, ukubwa wake pamoja na mambo mbalimbali ya kipekee yanayojitokeza miguuni. Waulize kama wana sehemu inayowapendeza miguuni.***

Mchezo

Fanya kiondoa ubaridi au mchezo unaoendana na kiini 'nyayo za miguu' . Hapa kuna mapendekezo kadhaa[1]:

1. **Mbinu:** Wachezaji wote au wana timu wanakaa pamoja na kujaribu kupeana vizibo kutoka jirani mmoja hadi mwingine kwa kutumia vidole gumba.
2. **Kuweka sawa maputo:** Kwa kutumia miguu tu, puto moja au zaidi yanatakiwa yawe angani bila ya puto kuruhusiwa kugusa ardhi. Hili zoezi linaweza likawekewa muda vile vile.
3. **Uwanja wa miguu bila viatu:** Vitu vya aina mbalimbali vinatakiwa vitambulike na mtu kwa kutumia miguu yake kugusa na kutambua hicho kitu huku akiwa kafumbwa macho.

***Waulize watoto na usikilize majibu yao:***
***Unafikiri nini unapofikiria kuhusu nyayo za miguu yako?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Leo tunaitizama hadithi ya Danieli inayopatikana katika Agano la Kale. Hadithi ya Biblia ya Danieli inaonyesha kujiamini, kujitoa na ujasiri wa vijana wanne wakati mgumu sana. Walichukuliwa mateka na mfalme Nebukadneza. Hadithi ya Biblia inaonyesha jinsi Danieli na marafiki zake walivyoacha nyayo kubwa za miguu katika maisha ya wengine – na hasa Mfalme Nebukadineza na Mfalme Dario – kwa kujitoa kwao kwa Mungu na kwa utumishi kwa wengine wakati mgumu sana.

## Hadithi ya Danieli

Tafuta njia ya ubunifu ya kuisoma hadithi ya Danieli pamoja na watoto. Huenda unataka kutumia Biblia maalum ya watoto au video ya YouTube. Uwe mbunifu uwezavyo! Katika somo tutazingatia sura ya sita.

***Hapa kuna mapendekezo kadhaa kwa ajili yako:***

1. **Vitabu:**

   - Daniel in the Lions'Den, The Brick Bible for Kids by Brendan Powell Smith, The Brick Bible Book Store

2. **Videos:**

   - Daniel in the Lions' Den
   - Daniel and the Lion's Den - Animated Scripture Lesson for Kids
   - VeggieTales - Daniel and the Lions' Den

1 https://www.youthwork-practice.com/games/feets-toes-legs-games.html

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Unaweza kujieleza ulivyo wewe mwenyewe kwa maneno matatu? Na maneno hayo ni yapi?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Huenda unajieleza kwamba wewe ni “Mcheshi, mwenye akili na mvivu’, lakini inaweza ikawa  ‘mpole, mwenye aibu na mwenye kusaidia’. Maneno yote haya yanaelezea tabia yako wewe. Tabia yetu inahusika sana na maisha yetu na mahusiano yetu.  Kama wewe ni mkweli, watu watakuamini. Kama wewe ni mvivu, hautaonekana kuwa ni mfanyakazi wa bidii.  Katika hadithi ya Danieli tunaona jinsi tabia yake ilivyogusa maisha ya watu waliomzunguka.

Dario alifanywa mfalme wakati yeye na majeshi yake yalipomshinda Belshaza na wakaingia Babeli ndani ya kuta. Kama mtawala wa eneo hili jipya, Dario alichagua magavana 120 wawe wenye mamlaka juu ya watu wanaoishi maeneo mbalimbali ndani ya himaya. Magavana hawa 120 walikuwa chini ya  uongozi wa wasaidizi wa rais watatu ambao walichaguliwa na mfalme.

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Maneno yapi matatu yanaelezea tabia ya Danieli?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

## Habari ya msingi kuhusu hadithi ya Danieli sura ya 6.

Danieli alikuwa na sifa nzuri sana mbele zake mfalme Dario, na kwasababu ya sifa yake nzuri mfalme alikuwa anapanga kumpandisha cheo na alikuwa anapanga kumweka juu ya ufalme wote.

Wale wasaidizi wa rais wawili hawakupendezwa na wazo hili la mfalme la kutaka kumpandisha Danieli awe mtawala mkuu wa ufalme wote. Walikuwa na wivu kwasababu mfalme alifikiri kwamba Danieli alikuwa mtu bora mwenye sifa za kipekee. Hawakutaka apandishwe cheo awe mkuu wa ufalme wote. Kwa bidii walitafuta makosa ya Danieli badala ya kuangalia mazuri yake.

Njia pekee ambayo ingeweza kumfanya Danieli asionekana wa maana machoni pa mfalme ilikuwa kupata jambo ambalo Danieli alikuwa analikosea katika kazi yake.  Je, wangeweza kumkamata akiwa sio mwaminifu kazini au akichukua fedha  ambazo sio za kwake. Huenda wangemkamata akiwa analala kazini wakati wa kazi. Walitafuta na kutafuta wapate jambo baya la kusema kuhusu Danieli lakini hawakupata kitu chochote kibaya. Katika kila jambo Danieli alikuwa mwaminifu.

Wakachanganyikiwa wale wasaidizi wawili wa rais kwamba hawakuweza kupata jambo lolote baya juu ya tabia ya Danieli.  Bado walitaka aonekana hafai mbele za mfalme kwa hiyo walifikiria wakaona njia pekee ya kumfanya Danieli aonekana mbaya ilikuwa kumfanya avunje sheria za Mungu.  Walijua kwamba Danieli alikuwa mwaminifu kwa Mungu wake na njia pekee ambayo ingemfanya akosee ilikuwa ni kumtendea dhambi Mungu.
Wale wasaidizi wawili wa rais wakawakusanya magavana wengi waliokuwa wanatumika katika ufalme wakawaambia mpango waliokuwa nao wa kumwangusha Danieli. Walikuwa na hamu kubwa sana ya kumwingiza Daniei katika makosa hivyo kinyume sana wakaanza kuwashawishi magavana. Walipokamilisha mpango wao na wakafaulu kupata watu wengi waliounga mkono huo mpango, wakaupeleka huo mpango kwa mfalme Daro.

Fikiria kama wewe ungekuwa mfalme Dario siku ambayo viongozi aliowateua walipokwenda mbele zake. Walisimama mbele zake wakasema maneno ya uongo. Walisema, 'Ewe mfalme Dario, uishi milele! Tumekaa pamoja tukakubaliana kwamba tunafikiri utengeneze sheria kwamba katika siku 30 zijazo mtu asimwabudu, asiombe mungu mwingine yeyote ila wewe. Kama mtu atavunja sheria hii adhabu yake itakuwa kutupwa katika tundu la simba.'

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Unafikiri mfalme Dario atajibu nini? Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti na useme: 'Hebu tuone jinsi mfalme Dario alivyojibu.'***

Mfalme alidanganyika. Hapa lilikuwepo kundi la viongozi lililokuwa linapendekeza kwamba watu wote wamwabudu yeye tu kwa siku 30. Lilionekana kama wazo zuri kwake kwasababu huenda alikuwa anafikiria jinsi itakavyokuwa vizuri kusifiwa na watu katika ufalme wake. Aliandika hiyo sheria na akaiwekea sahihi yake na mhuri wake na kufanya sheria isiweze kubadilishwa. Yaliyoandikwa lazima yakamilishwe na hakuna wa kuweza kubadilisha sheria ya mfalme.

***Waulize watoto: Unafikiri nini kina mguzo chanya katika mfalme Dario? Danieli au wasaidizi wawili wa rais? Kwanini unafikiri hivyo?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Wale wasaidizi wawili wa mfalme waliwaachia magavana na mfalme athari za kinyume: lengo lao lilikuwa kumuumiza Danieli na kumfanya atende dhambi dhidi ya Mungu. Danieli yeye aliacha mguso chanya; alimsaidia mfalme kwa kutumia sifa zake za kipekee.
Danieli aliposikia kwamba sheria imeandikwa na kuwekewa sahihi na mfalme alikwenda nyumbani akafanya alivyokuwa akifanya siku zote. Alifungua dirisha lake lililokuwa likielekea upande wa Yerusalemu, mahali alipoishi na watu wa Mungu miaka mingi ya nyuma. Akapiga magoti akaanza kuomba akimuuliza Mungu amsaidie. Danieli alikuwa mwaminifu kwa Mungu na hakuruhusu chochote kimzuie kuomba na kuzungumza na Mungu.

Danieli alipokuwa akiomba na dirisha lake likiwa wazi, wasimamizi na magavana walikuja nyumbani kwake wakamkuta anamwomba Mungu wake. Wakarudi haraka kwa mfalme Dario wakamwambia, 'Danieli, mmoja wa wakimbizi (mtu aliyechukuliwa kutoka katika nchi yao) kutoka Yuda hakusikilizi, Ewe mfalme, wala hatii sheria uliyoiweka kwa maandishi. Bado anamwomba Mungu wake mara tatu kwa siku.' Mfalme Dario alitaabishwa sana. Alijua Danieli alikuwa mtu mwaminifu mwenye roho safi. Alijitahidi sana kuzuia Danieli asiadhibiwe kwasababu ya kuvunja sheria hii. Alifanya kazi kwa bidii mpaka siku ikaisha akijaribu kumwokoa Danieli kutoka kwa adhabu yake.

***Waulize watoto na usikilize majibu ya: Unajisikiaje kuhusu mfalme Dario?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Umewahi kujisikia kama alivyojisikia mfalme Dario, akijutia tendo kwasababu linamuumiza mwingine?***

***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Wasimamizi na magavana walimrudia mfalme wakamkumbusha kwamba hawezi kuvunja sheria yake mwenyewe na kwamba Danieli lazima aadhibiwe kwenye tundu la simba.

Mfalme Dario hakutumia hekima alipotengeneza sheria yake hii. Alishawishiwa na watu waliotaka kumuumiza Danieli. Huenda alifikiria sheria hii itamfanya awe na furaha na ajisikie anapendwa. Lakini badala yake ilimfanya awe na huzuni. Alijua kwamba amefanya makosa. Na kwa sababu ya hilo Danieli sasa alikuwa anawekwa kwenye nafasi ya hatari. Akifahamu kwamba sasa hana chaguo jingine, Dario aliagiza Danieli atupwe kwenye tundu la simba. Danieli alipokuwa anapelekwa kwenye tundu la simba, mfalme alisema:‘Mungu wako, unayemtumikia daima, yeye atakuponya!’

Danieli alipotupwa kwenye tundu la simba mfalme aliweka jiwe kwenye mlango wa tundu na akaliwekea muhuri wa pete yake. Dario akarudi kwenye ikulu yake na usiku huo hakula wala hakujistarehesha kwa namna yoyote.

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Sijui ni jambo gani jingine alilolifanya Mfalme Dario usiku huo na alijisikiaje...***

***Angalia kote uone ni nani anayetaka kujibu na upokee majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Kwa kweli hatujui alifanya nini, lakini tunajua kwamba lazima ulikuwa usiku mrefu sana kwa Dario.

Mara kulipopambazuka Dario alikimbia kwenda kwenye tundu la simba. Alipofika kwenye tundu alimwita Danieli kwa sauti yenye huzuni, ‘Danieli mtumishi wa Mungu aliye hai, Mungu wako, unayemtumikia daima, ameweza kukuokoa na simba hawa?’ Alipata nafuu gani Dario kusikia Danieli akisema, ‘Ee mfalme, uishi milele. Mungu wangu amemtuma malaika wake naye ameyafumba makanwa ya simba, nao hawakunidhuru, kwa kuwa mbele zake mimi nalionekana kuwa sina hatia; tena mbele yako, Ee mfalme sikukosa neno.’

Danieli alikuwa analindwa na Mungu wakati wote! Endelea kumwamini Mungu, na kujitoa kwa kusudi lake na uwe jasiri katika nyakati ngumu. Kama ukiendelea kuungana na Mungu kila siku, kwa kumsikiliza, kuomba na kusoma neno lake, utapata nguvu kupitia kwa Roho Mtakatifu kama ilivyokuwa kwa Danieli.

Mfalme alifurahi sana kwamba Danieli alikuwa mzima! Akaamuru wamtoe Danieli kutoka katika lile tundu. Ndipo Danieli akatolewa katika lile tundu, wala dhara lolote halikuonekana mwilini mwake, kwasababu alikuwa anamtumainia Mungu wake! Mfalme Dario akaandika sheria mpya iliyosema kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wake watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli. Mfalme Dario aliona uwezo katika maisha mema ya Danieli na ulinzi wake kutokana na simba wenye njaa. Dario alimtukuza Mungu aliye hai mbele za watu.

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Ni nyayo gani ambayo Danieli aliacha katika maisha ya mfalme Dario? Au : Maisha ya Danieli yalikuwa na mguso wa namna gani kwa maisha ya mfalme Dario?***
***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Kujiamini kwa Danieli, kujitoa kwake na ujasiri viliwaathiri wale waliomzunguka. Tizama mguso ambao Danieli alimwachia Mfalme Dario!

***Waulize watoto na usikilize majibu yao: Unawezaje kuacha nyayo zako za miguu / unaweza kuacha mguso chanya kwa wengine kwa tabia, karama, na ujuzi wako?***

***Pokea majibu kwa kuyarudia au kuyasema kwa njia tofauti.***

Kama unajaribu kuwa mshawishi mzuri ni muhimu umuulize Mungu akuonyeshe kama una tabia au mazoea ambayo yanaweza kuwa sio mfano mzuri kwa wale wanaokutazama.
Kama bado hujaukubali upendo wa Mungu kwako na msamaha wake, basi kwa urahisi tu mwombe hayo na umwombe Roho Mtakatifu akusaidie.

Hebu tuchague kuishi maisha mema kati ya wengine ili tuwe taa kwa wengine na tumtukuze Mungu!

## Maswali ya kutathmini somo:

- Dario ni nani?
- Dario alikuwa na magavana wangapi katika ufalme wake?
- Kwanini wale wasaidizi wawili wa rais walikuwa na wivu juu ya Danieli?
- Kwanini walitafuta wapate kitu ambacho Danieli alikuwa amekikosea maishani mwake?
- Kwanini walipanga wa mwingize Danieli kwenye shida mbele za mfalme?
- Kwanini Dario alisikitishwa walipomwambia kuhusu kumwona Danieli anaomba?
- Dario alifanya nini usiku wakati Danieli alipokuwa katika tundu la simba?
- Danieli alilindwa namna gani alipokuwa katika tundu la Simba?
- Ungependa uwe mtu yupi katika hadithi hii na ni kwanini?
- Unafikiri sehemu muhimu sana ya hadithi hii ni ipi?
- Unaweza kufanya nini juma hili litakalokuwa na ushawishi chanya katika maisha ya mwingine?

Maswali haya yanatokana na Ministry to Children[1] na maswali ya ajabu kutoka katika mchezo wa Mungu 'Godly Play'[2]

**1** Ministry to youth - Daniel & the lions den (lesson activities)
**2** Godly Play UK – A Christian movement centered on childhood spirituality

# Kufuata mfano wa Danieli.

## Funguo za kuacha nyayo za miguu yako mahali ulipo.

### 1 Upendo wa Mungu

Upendo wa Mungu ni kwa ajili yako, upendo wake umekuzunguka. Mungu alimtoa mwanae wa pekee Yesu ili kila mtu amwaminie asipotee bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16). Kama unataka kuacha alama mahali ulipo, upendo wa Mungu ndicho kitu pekee unachohitaji. Upendo wake utakuwezesha kuwapenda wengine na kujipenda wewe mwenyewe. Ni upendo wake utakaokufanya uende umbali wa ziada ili uone kusudi la Mungu likitimizwa.

### 2 Neno la Mungu na Maombi

Ni muhimu kujifunza Biblia kwasababu Neno la Mungu linakuongoza katika mwelekeo sahihi maishani. Hukuangazia njia mbele yako ili uone wazi ni wapi pa kwenda. Kupitia kila msimu wa maisha yako, unaweza kuamini kwamba Mungu daima anakuongoza kupitia kwa Neno lake ( Zaburi 119:11).

Kujifunza Biblia hukupa moyo na nia ya Mungu kwa ajili ya maisha yako na kwa ajili ya watu wanaokuzunguka. Mungu hupendezwa kujibu unapoomba kutoka mahali hapa pa kuabudu katika Kristo na Neno lake. Danieli na marafiki zake walielewa nafasi ya neno la Mungu na maombi katika maisha yao na wakaendelea kumsikiliza Mungu katika mazingira yote.

### 3 Uwe umeuzwa kwa Mungu – Utii

Watu walioacha kwa kweli nyayo zao kama Nelson Mandela na Mama Teresa wana kitu kimoja cha kufanana: waliwatanguliza wengine badala ya kujitanguliza wenyewe. Kama unataka kuacha nyayo za milele, mwangalie Kristo na wengine na usijali nafasi yako, wadhifa au sifa zako. Danieli na marafiki zake walikuwa wameuzwa kikamilifu kwake Mungu nao waliishi kwa utiifu kwa kusudi lake katika maisha yao.

Danieli alimpenda Mungu kuliko kingine chochote, kwa hiyo alitaka kuendelea kuwa hajaachana na Mungu, bila kujali nini wengine walisema. Inahitajika upate mvulana au msichana mmoja tu ambaye kajitoa kuwa mtiifu kutumiwa na Mungu ili uweze kuigusa familia, jamii, shule, mji au hata taifa zima. Utiifu wa kawaida sana unaweza kusababisha yapatikane mambo ambayo huwezi kuyadhania.

### 4 Mtu wa Kiroho na mwenye nguvu

Kama Danieli, wewe unaweza kuwa umejaa Roho Mtakatifu na nguvu kama unataka kuweka alama isiyofutika kwa ushahidi usio na makosa.

## 5 Hekima ya Mungu

Hekima ni uwezo wa kupambanua na kutoa hukumu ni sehemu gani ya maarifa hayo ni ya kweli, sahihi, itakayodumu na inahusika na maisha yako. Kupambanua tofauti kati ya hayo mawili inaweza kuwa jambo gumu. Ili wewe uache nyayo zako popote ulipo, unahitaji hekima vile vile. Hakikisha una watu waliokuzunguka wenye hekima na watu wa kiroho watakao kusaidia kufanya maamuzi sahihi.

## 6 Familia ya kiroho

Kama Danieli, sisi nasi tunawahitaji marafiki wanaosafiri pamoja nasi, katika safari yetu ya imani. Hakikisha umezungukwa na marafiki wa kiroho na jamii ya imani yenye upendo. Watakusaidia wakati mgumu nawe utawasaidia wao!

**Kila mmoja anaweza kuleta tofauti kwa kubadilisha muundo wake wa tabia.**

**Wewe unawezaje?**

Jumuisha mapendekezo haya ili kupunguza nyayo zako za kawaida na ulete mguso chanya!

Punguza mara moja matumizi ya vitu kama plastiki za kutupa.
Ulikuwa unajua kwamba plastiki zote tulizotengeneza bado zipo?
Tunatumia mifuko ya plastiki kwa manunuzi kwa wastani wa dakika 12 kabla hatujaitupa (na ndiyo, bado kuna mifuko ya plastiki katika maduka ya nguo, vifaa vya ujenzi na sehemu nyingi mbalimbali ). Vifaa vingine vya plastiki vya kutumia na kutupa kama mirija ya kunywe soda, vikombe na sahani vinatumika kwa muda mrefu kiasi. Badilisha uanze kutumia vitu vinavyoweza kurudiwa kutumika, kama chupa za maji zinazoweza kutumiwa tena, mifuko inayoweza kutumiwa tena na vikombe vinavyoweza kutumika tena. Hatua nzuri ya kuanza nayo ni kila siku kataa kutumia plastiki kila unapoweza.

**Rasilimali zaidi**

1. Tembelea [http://www.myfootprint.org](http://www.myfootprint.org) ili kwa usahihi upime nyayo zako.
2. Tembelea [https://www.funkidslive.com/learn/what-is-a-carbon-footprint-and-what-can-we-do-to-reduce-it/](https://www.funkidslive.com/learn/what-is-a-carbon-footprint-and-what-can-we-do-to-reduce-it/) kama unataka kufahamu zaidi kuhusu nyayo zako za mkaa (carbon) na namna ya kuzipunguza!
3. Angalia mchezo wetu wa kadi ‘Imani Inayoongea’




# Ukweli kuhusu unyayo[1]

1. Katika mda wako wote wa kuishi, inawezekana ukawa umetembea kwa wastani maili 115,000. Hiyo ni kama kuzunguka dunia kwa miguu zaidi ya mara nne.
2. Kuna mifupa 26 kwenye mguu. Hiyo ni robo ya mifupa yote inayopatikana katika mwili wako. Kila mguu vile vile una viungo 33, mishipa 107 na misuli 19.
3. Unyayo wako unaweza kuwa sehemu inayotekenya sana katika mwili wako.

1 https://www.nyfoothealth.com/blog/2021/8/18/did-you-know-fun-facts-about-feet

# Mawazo ya kazi ya mikono

Tumeona jinsi  kujiamini kwa Danieli, kujitoa kwake na ujasiri wake ulivyowashawishi wale waliomzunguka. Na tumeona mguso wa Danieli kwa mfalme Dario! Aliacha nyayo za miguu za kipekee za sisi kufuata. Inaweza isiwe unyayo halisi wa mguu, lakini ni mfano ambao sisi sote tunaweza kuufuata. Ujiamini katika Bwana, uendelee kuwa umejitoa kwake Mungu na uwe jasiri katika mazingira yote.

Ungependa uache nyayo kama Danieli?

Hebu tuungane tunapotengeneza kazi za mikono zitakazo tukumbusha kila mmoja wetu kuwa na kujiamini, na kuendelea kujitoa na tuwe jasiri ili tuweze kuacha na sisi nyayo za miguu yetu.

## Wazo la kazi ya mikono 1



Vitendea kazi vinavyohitajika:

1. Karatasi kubwa nyeupe au kitambaa
2. Rangi mbalimbali
3. Kalamu kubwa (Markers)

Kama kikundi, mnaweza kutumia vifaa vilivyopatikana kutengeneza alama za mikono au nyazo za miguu kwenye katarasi kubwa nyeupe au kitambaa kwa kutumia rangi zilizopatikana. Baada ya michoro kufanyika, ruhusu ikauke.

Waulize watoto ni ujumbe gani au maneno ya msingi gani yanayoweza kuandikwa kando ya michoro. (Haya yanaweza kuwa 'Uwe wewe', 'Weka alama yako', 'Uwe jasiri' na kuendelea.) Jumbe hizo zitakuwa ukumbusho kwa kila mmoja aache alama chanya, au nyayo za miguu chanya katika dunia hii.

## Wazo la kazi ya mikono 2





Vitendea kazi vinavyohitajika:

1. Karatasi ngumu / karatasi ya kawaida
2. Mikasi
3. Kalamu kubwa / penseli / kalamu za rangi
4. Nyuzi

Kwa kutumia karatasi iliyotolewa, chora mkono au mguu wako kwa kutumia penseli. Ukisha maliza; tumia kalamu kubwa ya rangi kukuza mchoro wako wa penseli. Chora zile alama dhahiri zinazoonekana kwenye mkono wako au mguu wako kwani hizi zitaonyesha utambulisho au safari uliyoipitia. Kwenye kiganja cha mkono au mguu, andika jina lako, kwa mfano: 'Maria au 'Yakobo'.

Juu ya kila kidole andika maombi matano yatakayokusaidia katika safari mahali unataka alama iachwe. Hii inaweza kuwa kuongeza mafanikio katika masomo yako, michezo au ndoto ya kazi unayoiona mbele yako unapojifunza zaidi kumhusu Mungu kila siku. Unaweza kutundika huu mchoro darasani kwenu au nyumbani kama ukumbusho wako wa mara kwa mara na maombi.

## Nyumbani – jinsi gani kuacha nyayo za miguu katika jamii yako

Waalike watoto na familia zao waache alama chanya ya nyayo za miguu yao katika maisha ya wengine kwa kutumia baadhi ya mawazo haya ya huduma[1]:

1. Waonyeshe tabasamu watu kumi leo!
2. Andika kadi na uitume kwa yule anayehitaji kutiwa moyo.
3. Mabadiliko ya hali ya hewa: fikiria namna unavyoweza kuokoa nishati leo.
4. Tengeneza keki au biskuti za kuwapa wengine.
5. Mpe jirani msaada leo.
6. Mwalike mtu aje kula chakula cha jioni.




1 Mawazo haya yamechukuliwa kutoka kwenye 40acts.org
Tafadhali tembelea mtandao upate chati kuu ya ubaoni yenye mawazo mbalimbali ya huduma kwa familia!

# Somo la Biblia la familia

Kwa familia, umri mbalimbali

Wapendwa familia na watu wa rika mbalimbali na kutoka nyanja mbalimbali, Asante kufungua taarifa hii na kukubali kuwashirikisha wanafamilia yako imani au watu wengine unaoshirikiana nao katika maisha haya.

Masomo haya ya Biblia ya familia ni kwa ajili yako wewe kutumia katika mazingira ya nyumbani kwako au katika makundi madogo ya watu wa madhehebu mbalimbali. Unaweza kutumia masomo haya mwisho wa juma la siku ya kimataifa ya watoto na vijana kama somo linavyopendekeza, lakini uwe huru kulitumia somo wakati mwingine wowote unaokubalika na hali yako.

Tunaomba kwamba ubarikiwe, na kwamba uhusiano wako na Kristo na uhusiano wako na wengine ukue kwa kina na kwamba Mungu aufungue moyo wako hata zaidi kwa ajili ya watu wanaokuzunguka.

## Ijumaa | Utambulisho

### Tulia na uombe

***Baba, twaomba neno lako liwe taa ya miguu yetu na mwanga wa njia zetu.***
***Roho, twaomba utupe pumzi yako, ili tuwe hai na tusimame kwa miguu yetu.***
***Yesu, twaomba tutembee kwa kufuata nyayo zako katika yote tuyafanyayo na tuyasemayo.***
***Amina.***

### Neno Lililo Hai

***Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake; wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa.' (Zaburi 1:3).***

### Somo la Biblia

Tunapoandika somo hili la Biblia, dunia taratibu inaondokana na wakati wa kutisha, wa janga la UVIKO 19. Tahadhari za janga hili zilitutaka tupunguze mizunguko na tusikaribiane sana kijamii, watu wakazuiliwa kusafiri na pakawepo kufungiwa ndani. Hii ilimaanisha kwamba hatukuweza kuwashirikisha wengine habari njema ya wokovu kwa njia ambayo tuliifahamu. . Tulipata changamoto ya kutafuta njia zingine za kuweka alama katika maisha ya wengine na kuwashirikisha habari njema iletayo wokovu, amani na furaha kwa watu wote (Isaya 52:7).

Biblia inatumia mfano wa mti uliopandwa kando kando ya maji ili kuelezea mtu ambaye amezama katika neno la Mungu. Huo ndiyo mtazamo wake kutwa kuchwa. Yeye kwa makusudi huamua kulielekea neno la Mungu linaloleta uhai na mwanga naye hukataa kuwasikiliza watu waliojaa hukumu, kejeli na uongo.

Hapa kuna kweli kadhaa kuhusu mti. Huenda ukapata nyingine zaidi wewe mwenyewe!

- Mti ni mmea mkubwa unaoweza kuishi kwa miaka mingi.
- Mti una shina moja.
- Shina hushikilia matawi na majani.
- Mti husimama kwasababu ya mizizi yake ambayo imejificha chini ya ardhi.
- Mizizi huusaidia mti kwa kusafirisha maji na virutubisho ambavyo vinahitajika na mti ili ukue.

Mti hutegemea mizizi yake kuupa nguvu na afya yake. Na kwa matunda yanayotoka kwenye huo mti unaweza kuona jinsi mti ulivyo na afya na nguvu. Ndivyo ilivyo na sisi. Nguvu na afya ya mahusiano yetu na Yesu huonekana kutokana na kile tunachokifanya na kile tunachokisema. Hayo ndiyo matunda yetu.

Wakati mahusiano yako na Yesu ni imara, tunakuwa sio rahisi kuyumbishwa, vile vile kama mti wenye mizizi imara. Mizizi ya imani yetu hukua kwa kina ndani ya Yesu, kama Paulo alivyosema katika barua yake kwa Wakolosai:

***'Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika yeye, mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa, mkizidi kutoa shukrani.' (Wakolosai 2:6-7).***

Ushauri wa Paulo kwa watu wa Kolosai ni: hakikisha unatengeneza nafasi kwa ajili ya Mungu, kila siku. Utastawi: imani yako itakuwa imara, upendo wako utaongezeka na furaha yako itakua. Tunapokuwa mbele za Mungu, hatuogopi. Tutapokea yote ambayo Mungu anayo kwa ajili yetu. Dhoruba zinaweza kuja na kuondoka, lakini sisi tutabaki. Tabia ya kweli ya Mungu imefunuliwa ndani yetu.

***Katika Yohana 15: 5, Yesu anasema: 'Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi. Akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote." Yesu anasema kwamba tukiendelea kushikamana naye, tutazaa matunda.***

Matunda tunayozalisha ni nyayo zetu; tofauti tunayoifanya katika dunia hii. Matunda yetu yanaweza kuleta matokeo chanya katika maisha ya watu wengine.

## Shughuli na maswali kwa mazungumzo

- Angalia mti kwenye ukurasa unaofuata.
- Ni lini unajisikia kuwa karibu na Mungu? Andika majibu yako karibu na shina.
- Unawezaje kuleta mabadiliko katika nyumba yako, mtaa au jiji? Andika majibu yako karibu na tunda.
- Uwe na mazungumzo na kila mmoja kuhusu majibu.
- Kuombeana wenyewe kwa wenyewe.
-

Weka alama yako, ukijua Yesu atakuwepo kila hatua njiani!

## Changamoto kwa familia

Kama familia, mna changamoto ya kupanda mti. Mti huo unatakiwa kutunzwa na familia, kuhakikisha kuwa unanyunyiziwa maji na kulishwa mara kwa mara ili ukue. Mti ni ukumbusho wa utambulisho wako katika Kristo na tofauti unayoweza kuileta ulimwenguni kwa sababu umejikita katika upendo wake.

## Maombi

***Baba, mwenye neema na upendo zaidi. Tunakuja mbele ya kiti chako cha neema tukijua kwamba unatupenda, na kwamba uliahidi kamwe hutotuacha wala hutotupungukia.***
***Roho, tuongoze katika safari hii ya maisha, ili tuishi maisha yanayokufanya ujivunie sisi tunapoacha alama za nyayo zetu hapa duniani.***
***Yesu, tusaidie kutangaza jina lako na mafundisho yako katika yote tunayofanya na kusema.***

***Amina.***

# Jumamosi | Mwongozo

## Kutulia na Kuomba

***Baba, naomba neno lako liwe taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu.***
***Roho, naomba utupumulie, ili tuweze kuishi na kusimama kwa miguu yetu.***
***Yesu, tufuate nyayo zako katika yote tunayofanya na kusema.***
***Amina.***

## Neno Linaloishi

***'Umkabidhi Bwana njia yako, pia umtumaini, naye atafanya.' (Zaburi 37:5).***

Umewahi kuona au kutumia dira? Ni chombo ambacho kina maelekezo makuu manne: kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Inatumika kwa mwelekeo na itakusaidia kupata njia yako ikiwa utapotea. Umewahi kufuata GPS ukaishia kusikojulikana? Labda ulianza safari yako bila kuangalia vizuri ramani.

Mungu anaaminika zaidi kuliko dira au ramani za Google. Tukiandika anuani na tukaingia barabarani bila kumuuliza kwanza, tunaweza kubakia tukitamani tungehakikisha kama njia inaelekea tunakotaka kufika.

Katika kitabu cha pili cha Samweli, tunamwona Daudi akitiwa mafuta kama Mfalme wa Yuda. Daudi alikuwa amejua kwamba angekuwa mfalme kabla ya upako wake, na, kwa kifo cha hivi karibuni cha Sauli, ilionekana kama wakati mzuri wa kuchukua kiti cha enzi. Alikuwa tayari. Akamwuliza Mungu afanye nini kinachofuata:

***'Ikawa baada ya hayo, Daudi akauliza kwa bwana, akasema, Je niupandie mji wowote wa Yuda? Bwana akamwambia, Haya panda, Daudi akasema , Niupandie mji upi? Akasema Hebroni.' (2 Samweli 2:1).***

Daudi alikuwa na wazo zuri sana la mwelekeo wake, lakini alikuwa anamjua sana Mungu na haja ya mwongozo wa Mungu. Kwa hiyo alihakikisha mara mbili na Mungu, kuona kama kwenda katika moja ya miji ya Yuda ilikuwa wazo zuri. Mungu alithibitisha mwelekeo huu na hata akampa Daudi hatima ya kina sana: Hebroni.

Wakati mwingine unaweza kuwa na wazo zuri la uchaguzi unaopaswa kufanya. Nitaenda wapi chuoni? Nataka niwe sehemu ya kundi gani? Kama vile Daudi, mhusishe Mungu katika kila uamuzi unaofanya au kila hatua unayochukua. Na kumbuka: wewe ni mtoto wa Mungu, unapendwa na Mungu na sasa unaishi mbele za Mungu. Angalia kile Paulo aliandika kuhusu hili:

***‘Kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli;  mkihakiki ni nini impendezayo Bwana.’ (Waefeso 5: 9-10).***

Tunapoendelea kushikamana na Mungu tutafanya - hatua kwa hatua - kuelewa mwelekeo wa Mungu kwa maisha yetu. Uwepo wa Mungu ni kama nuru inayong’aa kwenye njia yetu. Pamoja na Mungu tunaweza kuhakikisha kwamba tunaenda njia sahihi, hata kama haieleweki kwetu.

Mungu ni mkuu sana kuliko sisi. Mungu peke yake anaona picha kubwa ya maisha yetu. Unapotembea na Mungu, unaweza kuamini mwelekeo wake, hata kama ni zaidi ya uelewa wako.

## Shughuli

**Mahitaji yanayohitajika**

- Kitambaa (kitambaa cha zamani kitafaa) au karatasi
- Kamba
- Mkasi
- Kalamu
- Gundi/kibanio/vibanio vya nguo

Kila mtu anaweza kutengeneza pembetatu yake. Andika kifungu chako ukipendacho upande mmoja na jibu la moja ya maswali hapa chini upande mwingine:

***Naamini Mungu ananiongoza kwenda wapi maishani mwangu?***
***Matamanio yangu kwa siku zijazo ni yapi?***

Tafuta mtu wa kuchanganya pembetatu zenu pamoja na mzitundike nyumbani kwenu / kanisani mahali ambapo wengine wanaweza kuziombea.



## Maombi

***Baba, mwenye neema na upendo zaidi. Tunakuja mbele za kiti chako cha neema tukijua kwamba unatupenda, na kwamba uliahidi kamwe hutotuacha wala hutotupungukia.***

***Roho, tuongoze katika safari hii ya maisha, ili tuishi maisha yanayokufanya ujivunie tunapoacha nyayo zetu hapa duniani.***

***Yesu, tusaidie kutangaza jina lako na mafundisho yako katika yote tunayofanya na kusema.***

***Amina.***

# Jumapili | Safari

## Kutulia na Kuomba

***Baba, naomba neno lako liwe taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu.***
***Roho, naomba utupumulie, ili tuweze kuishi na kusimama kwa miguu yetu.***
***Yesu, naomba tufuate nyayo zako katika yote tunayoyafanya na kusema.***
***Amina.***

## Neno Linaloishi

***"Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao." (Luka 24:15).***

Maisha yanaweza kuwa kama safari iliyojaa vituko. Nakumbuka safari yangu ya shule ya msingi tulipotembelea hifadhi ya wanyama. Sehemu ya kujifurahisha ilikuwa kupata mfuko wa mambo mazuri na kufurahi kwenye basi na marafiki zangu.Kuna neno la ajabu ambalo limekuwa likivuma kwa muda mrefu: 'kubwa kuliko wakati wote'. Mtu hupata cheo hiki kutokana na kutokuwa mzuri tu kwa kile anachofanya, bali kuwa MKUBWA, akimzidi kila mtu au kitu kingine chochote kinachomzunguka; kutoka kwa mwanariadha hadi gari. Kwa kawaida hufupishwa kama MBUZI." Yesu Kristo Nyota Mkuu' ni moja ya muziki mkubwa wa wakati wote, Albert Einstein mwanasayansi mkubwa, Lionel Messi mchezaji mkubwa wa mpira wa miguu na Nelson Mandela mmoja wa viongozi wakuu wa wakati wote.

Kinachomfanya mtu kuwa mkubwa kuliko wote ni rahisi. Anahitaji kufaulu katika safari yake ya maisha, hasa katika kipaji au ujuzi ambao Mungu amempa. Ni sawa kusema kwamba mkuu wa kweli wa wakati wote (kuanzia miaka 2,000 iliyopita) ni Yesu Kristo. Tunaangalia safari yake maishani: kuzaliwa katika hori, kukua ili kuonyesha ulimwengu upendo mkubwa zaidi ambao wangeweza kuupata, na kuonyesha kwamba sisi sote ni muhimu machoni pa Mungu.


Leo, tunapoangalia kifungu cha Biblia kutoka Luka, tunakumbushwa pia juu ya hamu ya Yesu ya kutembea nasi kila siku, bila kujali barabara tunayotembelea inafananaje. Unaweza kujisikia hauko salama wakati huu, kwa sababu ya changamoto kadhaa ambazo ziko mbele yako. Unaweza kuwa na msisimko sana juu ya matukio fulani unayokaribia kuyaanza.

Bila kujali safari yako inafananaje: Yesu atakuwa akitembea kando yako. Mkubwa kuliko wote wakati wote, yule mwenye nguvu kuliko kifo, atakuwa pamoja nawe. Hauko peke yako!

***Huyu ni July Ponce.***

Ana umri wa miaka 19.
Anatokea Peru na ni mwanachama wa Kikundi cha Kimataifa cha Ushauri wa Watoto na Vijana. Anasema yafuatayo kuhusu uhusiano wake na Yesu:

“Daima amekuwa nami na amenibariki kwa njia rahisi na nzuri zaidi. Namuona nikirudi nyumbani kutoka chuoni usiku nimechelewa nikiwa salama na salimini, ninapoamka na kusikia ndege wakiimba, au anaponipa fursa ya kupiga simu ya video kwa familia yangu. Ndoto yangu ni kuwasaidia vijana wengine kuwa karibu na Mungu na kuelewa kwamba kuwa na uhusiano na Mungu kunamaanisha kuwa na marafiki bora zaidi karibu yako.”




## Yazungumze

- ***Unajisikia kwamba Yesu yuko pamoja nawe lini?***
- ***Ni nani aliyekusaidia au aliyekufikia wakati ulipopitia wakati mgumu? Mwandikie kadi***

## Maombi

***Baba, mwenye neema na upendo zaidi. Tunakuja mbele ya kiti chako cha neema tukijua kwamba unatupenda, na kwamba uliahidi kamwe hutotuacha wala hutotupungukia.***

***Roho, tuongoze katika safari hii ya maisha, ili tuishi maisha yanayokufanya ujivunie tunapoacha nyayo zetu hapa duniani.***

***Yesu, tusaidie kutangaza jina lako na mafundisho yako katika yote tunayofanya na kusema.***
***Amina.***

# Milipuko ya maombi

**Kwa vijana**

Asante kwa kufungua taarifa hii! Kwa kufanya hivi unaonyesha kwamba maombi ni muhimu! Tumeunda miongozo minne ya kukusaidia katika muda wako wa maombi wakati wa Siku ya Kimataifa ya Watoto na Vijana. Sio lazima ufanye haya yote kwa mara moja. Chukua muda wako na uache Roho Mtakatifu akuongoze unapofungua Biblia yako na kuanza kuomba.

Kila kipindi kinachukua kama dakika 15 na kinajumuisha kusoma Maandiko, ibada fupi na mwongozo wa maombi.

Mada hizo ni kama ifuatavyo:

1. Katika Mungu
2. Kuwa wewe
3. Simama uonekane
4. Weka alama yako

Haya yameandaliwa kwa ajili ya vijana. Hata hivyo, hata kama wewe ni mwenye umri mkubwa kidogo, tafadhali uwe huru kutumia misaada hii.

## Mlipuko wa Maombi 1 | Katika Mungu

***'Uzielekeze hatua zangu kwa neno lako, Uovu usije ukanimiliki' (Zaburi 119:133)***

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watoto na Vijana 2023 ni 'Nyayo'. Tunaangalia alama tunazoacha nyuma, ushawishi ambao Mungu anao katika maisha yetu na ushawishi ambao Mungu anaweza kuwa nao kupitia katika maisha yetu au maisha ya watu wanaotuzunguka. Tunaanza nyakati hizi za maombi kwa kutafakari kuhusu Zaburi 119:133.

Hebu tuchukue muda na tutafakari juu ya tafsiri tofauti za mstari huu wa Biblia. Kila toleo linatupa ufahamu zaidi na kuthamini maandishi ya awali ya Mfalme Daudi. Tunapoangalia tafsiri tofauti, ninakualika ujisalimishe kwa Roho Mtakatifu na umpe nafasi ya kuangaza nuru yake ndani ya moyo wako. Jisikie huru kutulia na kutoa nafasi kwa chochote ambacho Roho anakufunulia.

### Zaburi 119: 133a

| | |
|---|---|
| King James Version | 'Agiza hatua zangu katika neno lako' |
| New King James Version | 'Elekeza hatua zangu kwa lako' |
| New American Standard Bible 2020 | 'Anzisha hatua zangu sawa na neno lako' |
| New International Version | 'Elekeza hatua zangu za miguu sawa na neno lako' |
| Amplified Bible | 'Anzisha hatua za miguu yangu kwa njia ya neno lako' |

Maneno ‘utaratibu’, ‘moja kwa moja’ na ‘kuanzisha’ hujitokeza tena na tena katika tafsiri tofauti. Utaratibu, moja kwa moja na kuanzisha. Unapoagiza chakula kwenye mgahawa, una lengo fulani akilini. Unaweza kuwa unatafuta kitu chepesi au kitu cha kukushibisha. Uamuzi wako unaweza kutegemea jinsi chakula kinavyoonekana, ladha, harufu au jinsi kitakavyokufanya ujisikie. Vyovyote ilivyo, unaagiza kile ambacho moyo wako unataka. Mungu ana hamu Fulani maalum juu ya uumbaji wake, na anaamuru hatua zetu zitimize mpango wake. Anaelekeza na kuanzisha hatua zetu kulingana na mapenzi na madhumuni yake. Mtume Paulo anatukumbusha katika 1 Wakorintho 12 kwamba sisi sote ni sehemu ya mwili wa Kristo na tuna majukumu maalum sana ya kufanya. Hakuna sehemu moja ya mwili huu ambayo ni muhimu zaidi kuliko nyingine. Wakati sehemu moja haiko vizuri, mwili wote huteseka. Mungu alituanzisha, akatuamuru na kutuelekeza sote katika wakati wa uumbaji wetu akiwa na kazi fulani maalum akilini na sote tunafanya kazi pamoja kwa ajili ya utukufu wake.

Unaweza kuwa unajiuliza Mungu aliamuru nini kwa ajili ya maisha yako. Wewe ni sehemu gani ya mwili wa Kristo? Kuna njia nyingi za kuhakikisha Mungu anasema wewe ni nani. Hebu tujaribu zoezi lifuatalo na tuone kinachojitokeza. Kumbuka kumpa nafasi Roho Mtakatifu anapokuongoza.

## Mimi ni Nani?

Fikiria kuhusu watu watano katika maisha yako. Wanaweza kuwa wana familia, marafiki, wenzio au wanafunzi wenzako shuleni. Wanaweza kusema nini kama ukiwauliza wakueleze kwa maneno matatu? Chukua muda na uandike kile ambacho wanaweza kukisema.

| Jina / picha | Wanaweza kusema nini? |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

Unafikiria nini juu ya kile walichokisema hivi punde? Je, walitumia maneno yanayofanana na hayo kukuelezea? Hii inakufanya ujisikie namna gani?

Ukiangalia kwa undani zaidi maneno waliyotumia kukuelezea, mada ya kawaida itaibuka. Maneno kama vile mlezi, mwanamikakati, mbunifu, mleta amani n.k. Kuna sababu ya Kimungu kwa nini mada hizi zipo. Hivi ndivyo tunavyotambuliwa na watu wanaotuzunguka na inafunua jukumu tunalofanya katika mwili wa Kristo, kama Bwana alivyoagiza. Kama vile jicho haliwezi kujizuia kuona na pua haiwezi kujizuia kunusa, ni katika asili yetu kuishi maisha yetu kulingana na jukumu letu katika mwili wa Kristo. Hebu tusimamie hapa na tulipeleke hili kwa Mungu.

## Omba

***Mungu, ninapotafakari juu ya kile ulichoagiza kupitia kwenye maisha yangu, ninagundua ________________________kunihusu mimi. Fungua masikio yangu nisikie jinsi unavyotaka niwe katika ulimwengu wako, kama ulivyoagiza. Naingia ndani yako sasa, Bwana. Amina.***

Fungua moyo wako, akili na roho yako na upokee hekima kama Roho Mtakatifu anavyokuzungumzia. Anasema nini? Wewe ni nani?

**Kifungu cha Bible 1**

***'Waefeso 2:10 "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.'***

Waefeso 2:10

Kama vile jua linavyochomoza lisijipashe joto lenyewe na mto hutiririka maji sio kujiondolea kiu wenyewe, Mungu alituumba kipekee kwa kusudi maalum. Alituumba kama tulivyo na kutuelekeza mahali anapotaka tuishi kwa kudhihirisha kusudi lake. Pale anapotuweka, kuna neema, pana upatikanaji wa mahitaji na amani. Yesu anatukumbusha kwamba:

**Kifungu cha Bible 2**

***'Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote.'***

Yohana 15:5

Vipaji, muda, rasilimali, mahusiano, elimu, uzoefu na nafasi zetu ni mafuta kwa maisha yetu. Wakati mwingine mambo haya yanaweza kusababisha tujifafanue nje ya kile ambacho Mungu aliagiza. Hebu tuchague leo kukaa ndani ya Kristo na tuwe watu wa aina gani na tuwe kile ambacho Mungu anasema. Hapo tu ndipo tunaweza kufikia malengo ya milele tuliyoumbiwa.

Ninakualika utumie dakika chache zijazo kumwelekea Mungu na umwombe aongoze nyayo zako unapoendelea kuwa wewe, ndani yake.

## Omba

***Bwana, asante kwa kunitafuta wakati ninapoanguka kutoka kwenye mzabibu wa kweli. Nisaidie kukaa ndani yako ninapojitahidi kuwa yule uliyenifanya niwe. Naomba nibaki ndani yako na wewe ndani yangu ili niweze kuzaa matunda mengi. Nakushukuru Bwana. Amina.***

# Mlipuko wa Maombi 2 | Kuwa Wewe

***'Elekeza nyayo zangu kulingana na neno lako' (Zaburi 119 : 133)***

Umewahi kuwa na mawazo ya namna hii juu yako mwenyewe?

- 'Sina uerevu wa kutosha.'
- 'Sina uzuri wa kutosha.'
- 'Sina nguvu za kutosha.'

Kuna ushindani mwingi katika dunia hii. Kuna ushindani mzuri, kama kipindi cha runinga cha kufurahisha ambacho watu hushindana kwa tuzo ya kipuuzi au kwa kutoa mchango wa hisani, au wakati unacheza michezo na marafiki zako. Lakini pia kuna ushindani usio mzuri; unapojisikia hamu ya kufaulu katika kila kitu, kazini, shuleni n.k.

Ninapoangalia Facebook au Instagram, naona watu ambao wametengeneza nywele zao vizuri zaidi, wanafanikiwa zaidi na wametembelea maeneo mengi ya kigeni kuliko mimi. Nionapo machapisho hayo, ninajaribu sana kujilinganisha nao: 'Natamani ningekuwa mahali pao!'

Ushindani na kujilinganisha kunaweza kusababisha wasiwasi na msongo wa mawazo. Huwa tunashindana na kujilinganisha na wengine ambao wana kasi, ni nadhifu au wenye nguvu kuliko sisi. Matokeo ya mwisho: tunajisikia vibaya na kujifikiria: 'Hatutoshei.'

Leo tunakusherehekea wewe! Kuna mmoja wenu tu, hata kama wewe ni pacha. Sisi sote 'tumeumbwa kwa namna ya ajabu', maalum na ya kipekee. Watu wengine wana macho ya bluu, wengine wana macho ya kahawia, wengine wanaweza kufanya hivyo, watu wengine wanaweza kufanya hivi, watu wengine ni watumiaji wa mkono wa kulia, watu wengine ni wa mikono wa kushoto. Na unajua nini? Wewe ni kiumbe wa ajabu wa Mungu!

***"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo.' (Waefeso 2:10).***

Wewe ni kiumbe wa ajabu wa Mungu naye amekuandalia mambo mazuri ya kufanya. Kwa hiyo, Mungu ana mpango na wewe! Paulo anajaribu kuonyesha maana yake wakati unapozaliwa mara ya pili katika Kristo Yesu:

***"Basi kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndiyo kifungo cha ukamilifu.' (Wakolosai 3: 12-14 ).***

Ni kama Mungu alibadilisha kabati lako la nguo. Kuanzia sasa, unavaa soksi za huruma, mashati ya wema, suruali ya unyenyekevu, mkanda wa nguvu na koti la nidhamu. Lakini muhimu zaidi: msingi wako (chupi!) ni upendo, wakati wote! Upendo ule ule uliomleta Yesu katika ulimwengu huu, kuponya watu na kushinda kifo sasa unatiririka kupitia mishipa yako kama mtoto wa Mungu. Kubali utambulisho huu na utakuwa toleo bora zaidi la wewe mwenyewe!

***“Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.’ (Wagalatia 5: 25-26).***

Usijaribu kuwa mtu mwingine; kuwa wewe! Hii haimaanishi kwamba huwezi kujiboresha au kukua. Ukuaji ni sehemu ya mpango wa Mungu, na kwa hakika tunaweza kujifunza kutoka kwa wengine na kuiga vitendo na mitazamo bora. Lakini kuwa makini katika kujilinganisha na wengine. Ridhika na ulivyo. Kila mmoja wetu amefanywa mkamilifu kwa mfano wake kwa kusudi lake. Kwa kuwa mungu alitukusudia, tunaweza kuweka alama yetu!

## Wazo la Maombi

***Mimi ndivyo nilivyo kwa neema ya Mungu. Nitakuwa kile ambacho Mungu aliniumba na nitatimiza mpango wake kwangu.***

# Mlipuko wa Maombi 3 | Simama uonekane

***“Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.’ (Warumi 12: 2).***

Moja ya pongezi kubwa unayoweza kupokea ni kuambiwa kuwa wewe ni wa tofauti. Hii inaweza kuonekana kuwa kinyume na nyakati ambazo unataka kuwa sehemu ya kundi fulani la watu na kujaribu kuwa sahihi kabisa. Au unapotaka kuwa mwerevu, mtu poa, mwenye akili, ujuzi na kipaji kama wengine. Paulo anatukumbusha kwamba kama watoto wa Mungu, tunaweza kutegemea Roho wa Mungu kutubadilisha kutoka ndani kwa kutufanya upya mawazo yetu. Matokeo yake, tutaweza kutambua mapenzi ya Mungu ni yapi na kile ambacho Mungu anaona ni kizuri, cha kupendeza na kikamilifu.

Paulo anaelezea hili maana yake ni nini:

***“Kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu, katika kukaribisha wageni, mkijitahidi. Wabarikini wanaowaudhi, bariki wala msilaani. Furahini pamoja nao wanaofurahi, lieni pamoja nao waliao. Mpatane nia zenu ninyi kwa ninyi. Msinie yaliyo makuu, Lakini mkubali kushughulishwa na mambo manyonge. Msiwe watu wa kujivunia akili.’ (Warumi 12: 13-16).***

Unaona nini kinachokufanya uwe tofauti? Ni jinsi unavyofikiri! Sio ujifikirie mwenyewe tu , bali wafikirie na wengine! Roho ya Mungu itakuza upendo ndani yako ambao huenda zaidi ya ufahamu wako. Itakuwezesha kujipenda na kuwapenda na kuwatumikia wengine kwa namna ya pekee. Hivyo ndivyo unavyojitokeza!

Hakuna mtu mwingine katika ulimwengu huu ambaye ni sawa na wewe. Wewe ni mmoja wa aina yake! Upekee wako unatoka kwa Mungu.  Kumbuka kile Paulo aliandika kuhusu hili katika barua yake kwa Wagalatia:

***“Tukiishi kwa Roho, na tuenende kwa Roho. Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana. ‘ (Wagalatia 5: 25-26).***

***Kwa nini ni muhimu kwako kujitokeza?***
Tunataka kukupa changamoto ujionyeshe kuwa wa kipekee. Usiwe mwigizaji wa mtu mwingine. Usiwe mtu wa hisia, mbinafsi, mwenye kiburi. Uwe anayesimama kwa sababu ya huruma na wema wako!

Kwa kusimama uwe tofauti, unakuza upekee wako na unaleta utukufu kwa Mungu. Unawaelekeza wengine kwa Yesu. Unawaelekeza kwenye maisha ya matumaini, furaha na ukombozi kutoka kwa dhambi. Au kufafanua maneno ya mwana muziki Mary Mary, ondoa pingu miguuni mwako ili uweze kucheza. Kuwa mcheza densi anayehamasisha wengine kujiunga na ngoma hiyo. Hivyo ndivyo Mungu anavyotaka uwe.

***Unawezaje kuwa wa tofauti?***
Tunaweza kuwashawishi wale wanaotuzunguka kwa njia nzuri, si kwa kuwa kivutio kikuu, lakini kwa njia ya 'matunda ya kila siku ya Roho ya matendo yetu' . Kwa kuwapenda wale wanaotuzunguka, kuwa na furaha katika hali yoyote ile, na kuleta amani. Sisi ni nguzo kwa wale walio gizani karibu nasi. Tunasimama tukiwa tofauti.

Pia utasimama kutoka kwa umati kwa kuchagua mara kwa mara kufanya mambo ya kawaida kwa njia ya ajabu na isiyo ya kawaida kwa msisimko mkubwa. Msisimko na shauku vinaambukiza. Watu huvutiwa na wewe unapokuwa na furaha kuhusu maisha.

***Unaendeleaje kuwa wa tofauti?***
Wakati mwingine kuwa sehemu ya kikundi kunamaanisha kuendana na maadili ya kikundi. Na wakati mwingine hii inamaanisha kwamba upekee wako uko hatarini. Kwa hivyo, msingi wa uchaguzi wako uwe juu ya Neno la Mungu na uongozi wa Roho wake. Ungana na familia yako ya kiroho na marafiki ambao unawaamini na ambao wanaonyesha wema wa Mungu katika maisha yao. Kisha kwa hakika utakuwa wewe, katika Mungu, na utasimama ukiwa wa tofauti!

## Tendo la Maombi

Utahitaji yafuatayo:

- Karatasi
- Kalamu
- Pangi ya maji ya kung'aa
- Brashi ya kupakia rangi
- Vijiti vya kiberiti

Andika chini kitu ambacho kimekuzuia kuwa toleo bora zaidi la wewe mwenyewe na likakuongoza kusalimu amri. Inaweza kuwa kitu unachobeba moyoni na rohoni mwako, tukio la zamani ambalo lilibadilisha jinsi unavyoyaona maisha, au uzoefu ambao ulikubadilisha kabisa na kufanya safari yako na Mungu isivumilike na ikawa ngumu. Iwashe (salama na kusimamiwa ikiwa bado hujafikisha miaka 18) na uombe kwamba Mungu aibebe (Zaburi 55:22).

Zipake njiti za kiberiti rangi inayokuvutia zaidi na uiweka kama ukumbusho kwamba umetupa mizigo yako yote kwa Bwana ili uweze kuendelea na safari yako nyepesi na isiyo na mzigo. Anza tena, wakati huu na Mungu kama dira yako na lenga kusimama katika yote unayoyafanya. Acha rangi unayoichagua ikukumbushe kusimama na kukumbuka:

***'Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima.' (Mathayo 5:14,).***

## Changamoto

Huhitaji kuwa mtu maarufu au kushikilia nafasi kubwa ili ujitokeze. Tengeneza alama yako kwa kuwa na mchango kwa wale wanaokuzunguka. Mungu aendelee kutengeneza tabia yako na matendo yako yote. Kaa ndani ya Mungu, uwe wewe na usimame wa tofauti.

# Mlipuko wa Maombi 4 | Weka Alama Yako

***'Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi, nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mwombalo Baba kwa jina langu awapeni. Haya nawaamuru ninyi, mpate kupendana.' (Yohana 15:16-17).***

Hongera! Umefika umbali huu katika safari yako. Safari zetu zote ni tofauti, hivyo siwezi kuanza kuelewa safari yako ikoje. Je, ni rahisi? Imejaa shida? Leo tutaangalia safari yetu na namna tunavyoweza kuzaa matunda.
Au kwa maneno mengine: jinsi tunavyoweza kuweka alama yetu.

Tunapoangalia maisha ya Yesu, tunaona kwamba yote yalikuwa juu ya kuwatumikia wengine. Katika miaka mitatu alitembea kupitia Galilaya na Yuda, akiwafundisha wanafunzi na umati wa watu, akifanya miujiza na kuwakemea viongozi wa kanisa. Bila shaka aliweka alama yake!

Ukienda Israeli leo, unaona watu wanaofatilia hatua zake. Wanajaribu kufikiria hata zaidi maana ya kumfuata Yesu katika maisha halisi. Na Yesu si mtu pekee anayefuatwa na kuangaliwa kwa karibu sana. Maisha ya Nelson Mandela pia yanaangaliwa kwa karibu sana. Watu hutembelea ikulu ya rais au kisiwa cha Robben ambako alizuiliwa gerezani. Na kuna zaidi. Fikiria tu kuhusu Anne Frank, Rais Lincoln au William na Catherine Booth. Je, unajua wanaojitolea ndani ya Jeshi la Wokovu huwapeleka watu ziara Mwisho wa Mashariki wa London, wakifuatilia hatua za waanzilishi wetu na kuziishi siku za mwanzo za Jeshi la Wokovu?

Fikiria kuacha alama nzito kama hiyo duniani.
Neno nyayo linaweza kutumika kwa njia nyingi. Katika uchunguzi nyayo inaweza kuwa ushahidi katika eneo la uhalifu. Katika akiolojia, nyayo zimepatikana zikiwa zimehifadhiwa zikiandika maisha ya awali. Katika ulimwengu wa dijitali, tuna alama ya dijiti ambazo kwa kawaida tunaziacha bila kukusudia ambazo zingeweza kutufungua tuelewe hatari za utambulisho. Na kisha kuna alama yetu ya kiikolojia au kaboni ambayo inatusaidia kuelewa athari zetu kwa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa.

Sote huwa tunaacha mtiririko wa nyayo nyuma yetu popote tunapokwenda kulingana na jinsi tunavyoishi maisha yetu. Hebu fikiria juu yake kwa dakika moja. Unaacha alama gani nyuma? Je, ni alama ambayo wengine wanapaswa kuifuata, na kuishi nyayo zako? Au labda ni njia yenye ishara ya 'hatari' karibu nayo kwa sababu umefanya mambo ambayo yalikuwa na madhara kwako mwenyewe au kwa wengine. Haijalishi nyayo zako zilivyokuwa, kila nyayo mpya unayoiacha inaweza kuwaelekeza wengine kwa Yesu. Unachagua nyayo zako kwa misingi ya mapenzi?

Ni upendo huu ambao ulimfanya Yesu ayatoe maisha yake kwa ajili ya wengine (Yohana 15: 9-10; 12-13). Na je, uko tayari kuziishi hatua zake za upendo? Ni upendo huu wa ziada unaofungua mioyo yetu kupenda sio tu watu ambao wanastahili upendo, lakini kila mtu, pamoja na maadui zako.

Usiwe na mashaka! Unapomruhusu Yesu kukuongoza na unapomruhusu kuwa chanzo chako cha hamasa, safari iliyo mbele yako itakuwa na mvuto halisi. Haitakuwa rahisi kila wakati, lakini itakuwa na thamani. Na hausafiri peke yako!

## Changamoto

Hebu tufikirie nyayo zetu wenyewe kwa muda mfupi. Ikiwa unatumia mitandao ya kijamii, je, maoni, ujumbe na picha zako zinaonyesha njia ya Yesu? Nyayo zako za mitandao ya kijamii zinaonekanaje? Na katika 'ulimwengu halisi'? Unawaambia nini watu wanaokuzunguka? Matendo yako yanamwakisi vipi Yesu?

Tuna nafasi ya kuhamasisha  na kushawishi wengine kuishi maisha ya Kimungu. Tuna nafasi ya kubadilisha ulimwengu huu na kuuendeleza Ufalme wa Mungu

***Fikiria juu ya haya:***

- Mungu ameweka nini moyoni mwako?
- Unahisi umeelekezwa wapi kuweka alama yako?

Tembea katika nyayo zilizowekwa katika Neno la Mungu. Roho wa Mungu akutie moyo na akuongoze.

## Maombi

Mungu, naomba uelekeze hatua zangu. Naomba nitembee kwa namna inayokupendeza. Linda moyo wangu usikie kutoka kwako. Hamasisha matendo yangu yaweke alama inayowaleta watu katika Ufalme wako.

# Muhtasari wa Ujumbe 'Nifuate mimi!'

## Utangulizi na Ukaribisho

Kama una karatasi hii mkononi mwako, ina maana kwamba umebeba dhamana ya ujumbe wa Siku ya Kimataifa ya Watoto na Vijana. Hongera!

Katika muhtasari huu unaweza kupata habari ya msingi na vielekezo vinavyoweza kukuwezesha utengeneze ujumbe wako. Wewe ni mtu wa kipekee na Mungu anazungumza nawe kwa njia ya kipekee. Kwa hiyo ufanye ujumbe huu uwe wa kwako mwenyewe kwa uusoma na uusikilize kwa makini ujue kile ambacho Mungu anakisema.

Furahia safari hii na Mungu na ubarikiwe nayo na uwe Baraka kwa wengine!

## Natengenezaje ujumbe?

1. Chukua muda usome Kifungu cha maandiko kwa njia ya maombi. Fanya hivyo mara kadhaa na utumie tafsiri mbalimbali za maandiko. Nini kinakugusa? Una maswali gani? Nini kinakupa changamoto? Mungu anakwambia nini? Yaandike hayo chini.
2. Soma habari ya msingi. Habari hii inagusa namna gani uelewa wako wa vifungu vya Biblia? Ongeza mawazo yako hapo.
3. Fikiria kuhusu watu unaozungumza nao. Wao ni akina nani? Wanatokea wapi? Wana umri gani? Wanahitaji nini? Unaweza kukitumia kikundi cha watoto na vijana ujumbe wa kwenye mtandao. Watake wasome vifungu vya Biblia na wakufahamishe wana maswali gani na nini huwapa changamoto. Habari hii kila mara huwa ya msaada sana na bila shaka itakupa mwelekeo mzuri wa ujumbe wako.
4. Unataka watu waondoke na ujumbe upi? Andika hilo kwa sentensi moja.
5. Jitahidi kuzingatia vipengele moja hadi tatu katika ujumbe wako. Uwe huru kuchagua wa kwako, lakini hapa kuna mfano:

    a. Kuona– Zingatia kile ambacho Yesu anaona ndani ya wanafunzi wapya na kile akionacho ndani yetu.
    b. Kufuata – Zingatia ilimaanisha nini wanafunzi kuacha yote na kumfuata Yesu. Ina maana gani kwetu kumfuata Yesu?
    c. Kuvua –Zingatia maana ya maneno ya Yesu kuhusu uvuvi wa watu. Hiyo ina maana gani maishani mwetu?

6. Unaweza kufunua vipengele hivi vitatu kwa habari na maswali uliyokuwa nayo mwenyewe au uliyoyapata kutoka kwa kikundi cha vijana.
7. Malizia ujumbe wako kwa maswali ya kipekee yanayotoa changamoto kwa watu:

    a. Sijui ni sehemu gani ya hadithi hii inakuhusu?
    b. Sijui ni sehemu gani ya hadithi hii ni ya muhimu zaidi?
    c. Sijui kipi kinakupa changamoto kubwa zaidi katika hadithi hii?

8. Waalike watu wajibu kwa njia zao juu ya nini Mungu anasema nao. Je, Mungu anataka ajitoe upya? Mungu anawapa changamoto watu wafanye jambo fulani? Elezea kuhusu mahali pa kiti cha rehema na uwaalike watu wakitumie kiti cha rehema kama mahali pa maombi, wakijitoa au wakifanya upya kujitoa kwao.

## Maandiko –Mathayo 4:18-22

***'Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. Akawaambia, nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.***

***Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili, Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwemo chomboni, pamoja na Zebedayo baba yao, wakizitengeneza nyavu zao; akawaita. Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata.'***

# Habari ya msingi

(inapendekezwa isitumike kwenye ujumbe)

## Picha kuu na Mathayo

Hii lazima iwe ni hadithi muhimu kama ilivyoelezwa katika injili ya Marko (Marko 1:16-20), Luka (Luka 5:1-11) na inakuwa tofauti kidogo katika injili ya Yohana (Yohana 1:35-44). Waandishi wote wa injili waliamini ilikuwa muhimu kuwafanya wasomaji wafahamu jinsi safari ya wanafunzi 12 ilivyoanza, jinsi walivyopiga hatua zao za kwanza pamoja na Yesu. Na Mathayo anaielezea hadithi hii hata kabla ya ujumbe wa kwanza wa Yesu, ujumbe maarufu wa mlimani katika sura ya 5-7.

Kama utaingia katika kitabu cha Mathayo, unaona kila analolisema na kulifanya Yesu linaelekeza kwa ulimwengu mpya wa Mungu; ufalme wa Mungu. Unaliona hilo katika mifano, hadithi kuhusu mbegu ya haradari, kuhusu chachu na ujumbe wa mlimani wenyewe. Wakati Luka anawalenga wasikilizaji wa Kiyunani, Mathayo analenga jamii ya Wayahudi na anawaambia uhuru ni kwa wote. Huhitaji kupitia kwenye matambiko yote na ufuate kila aina ya sheria. Inapatikana kama maji mtoni (Mathayo 3). Katika Mathayo, lakini sio tu katika Mathayo, Yesu anaugeuza ulimwengu miguu juu kichwa chini. Na sisi sote tunaweza kuwa sehemu ya ufalme huo wa miguu juu na kichwa chini.

## Kuhusu wanafunzi

Kwa hiyo yeyote anaweza kuwa mfuasi wa Yesu? Yesu anatuonyesha jibu la swali hili kwa kuwa makini anamchagua nani. Sio kwa mara moja. Naona hii inaweza kuchanganya kidogo, lakini sivyo. Hebu nieleze kwanini.

Haikuwa jambo la ajabu katika desturi ya Wayahudi rabi kuwaalika wanafunzi wafuate nyayo zao. Ilichukuliwa kuwa ni heshima kubwa kama mtoto wako mmoja angechaguliwa kumfuata rabi na ajifunze nini maana ya kuwa mwanafunzi wa Kiyahudi au mwalimu. Katika jamii ya Yesu ilikuwa moja ya heshima za juu iliyotolewa tu kwa vijana wa daraja la juu.

Kwa hiyo, sio ajabu kwamba wanafunzi wa Yesu walimfuata mara moja baada ya yeye kuwaomba wafanye hivyo. Ilikuwa heshima kubwa kumfuata rabi! La ajabu ni kwamba hawa walikuwa wanaume sio vijana wa kiume. Jinsi unavyokuwa na umri mkubwa ndivyo ilivyo vigumu kujifunza, kwa hiyo ilikuwa ni chaguo la kipekee la Yesu kuwachagua wanaume wenye umri mkubwa.

Jambo jingine la kipekee ni kwamba Yesu aliwachagua watu waliokuwa na kazi zao. Walikuwa wavuvi. Njia yao ilikuwa wazi. Ilikuwa wafuate nyayo za baba zao. Unapokuwa mvuvi, utakuwa mvuvi siku zote.

Inawezekana Yesu alitaka dunia ijue kwamba yeyote anaweza kufuata nyayo zake? Nyayo za miguu yako haziko katika hali isiyoweza kubadilika. Unaweza kuchagua kumfuata Yesu wakati wowote, mahali popote, bila kujali historia yako, makuzi yako au kabila lako. Hii ni kwa yeyote, hata wale wavuvi wa chini.

Mara wavuvi walipoanza kumfuata Yesu, utambulisho wao ulibadilika. Hawakuendelea kuwa wavuvi tena, badala yake wakawa wanafunzi. Kwa hiyo mwanafunzi ni nani? Tunaigeukia kamusi ya Oxford tupate jibu:

***'Mmoja wa wale waliomfuata Yesu Kristo na mafundisho yake wakati alipokuwa akiishi hapa duniani, hasa mmoja wa wale kumi na wawili'***

Kutoka wakati huo na kuendelea, walisikiliza mafundisho ya Yesu, wakashuhudia miujiza yake, wakala naye, wakatembea na kuzungumza naye. Wakajifunza namna ya kumpenda Mungu, Baba yetu na namna gani kuwapenda wengine. Kwa kweli wanafunzi walifuata nyayo za Yesu kwenda kwenye harusi, kwenda mlimani, kwenda ziwani na kwenda kwenye miji mingi, kwenye nyumba na kwa watu wengi.

Ina maana gani kwetu kufuata nyayo za Yesu? Hatuwezi kufanya hivyo kama wanafunzi walivyofanya miaka zaidi ya 2,000 iliyopita. Lakini tunaweza kujifunza kutokana na mafundisho yake na tuishi maisha ya mtoto wa Mungu, vile vile kama yeye. Biblia inatuonyesha mafundisho mengi ya Yesu na wanafunzi wenzetu (wakristo) wanaweza kutushirikisha hadithi za namna gani wanavyomfuata Yesu. Umewahi kugundua kwamba Yesu alichagua wanafunzi 12 hapo mwanzo? Na kwamba kundi hili la wanafunzi likaendelea kukua na kukua? Kwa kweli Yesu anataka tusafiri pamoja na wafuasi wengine. Kwa hiyo kaa karibu na wale wanaokuonyesha namna na kumfuata Yesu. Na ukae karibu na Yesu mwenyewe kwa kupitia kwa maombi na kuwa na wakati wa upweke. Kama kwa kweli unataka kuona Yesu anataka kukuongoza wapi, unatakiwa uwe karibu naye!

## Maswali

Kuna maswali machache katika hadithi hii. Huenda unaweza kuwaachia wasikilizaji maswali machache yawafikirishe:

- Sijui ungefanya nini kama ungekuwa mmoja wa wavuvi hao?
- Sijui kama Yesu amewahi kukutaka umfuate?
- Sijui ulijibu nini kwa swali hilo?
- Sijui inafananaje kuzifuata nyayo za Yesu katika mazingira yako?
- Sijui kama unaweza kumfuata Yesu bila ya wafuasi wengine au wanafunzi wengine?

Uwe huru kuchagua baadhi ya maswali haya, lakini huenda ulipokea maswali kutoka kwa vijana wanaokuzunguka au una maswali ya kwako mwenyewe.

Naomba ubarikiwe wakati wa kujiandaa na ujisikie kuwa huru kuwashirikisha wengine ujumbe wa Yesu kwa uhuru.

***Kapteni Marc Potters***
***Afisa wa Kimataifa wa Watoto na Vijana***

# Wimbo A

***Nyayo za Miguu***

***[Ubeti wa Kwanza]***
Tumefika umbali huu
kutoka  kuwa wa pembeni
hadi kuweka viwango
Sauti zetu zilisikika nje ya nchi na  mbali
Mkono kwa mkono tutaiona siku bora
Tukiacha alama, nyayo zetu hupeleka ujumbe
Hatuhitaji kusema, Bwana amenena
Hatuna haja ya kuogopa, minyororo imevunjika

***[Pambio]***
Wabarikiwa ni
Wale wanaofuata
Maelekezo ya Mungu safarini
Acha hatua zako
Siku zote ziongozwe
Kwa Neno Linalonenwa na Mungu kila siku

***[Ubeti wa Pili]***
Sasa wakati umefika
Endelea mbele, simama imara,
Chagua kweli, na uepuke uongo
Tunaacha nyayo zetu, mchana na usiku
Bwana, upo upande wetu siku zote
Nguvu zako takatifu hutusaidia kupigana
Tunahitaji kuamini tu, Bwana anaongoza
Tunahitaji imani tu, Bwana anahudumia

# Wimbo B

***Nyayo za miguu***

***Ubeti wa Kwanza***
Wewe ni Mungu
Wewe ni Mungu
Sifa zote ni kwako

Wewe peke yako
Ndiye Kweli
Njia na Uzima

Unatuongoza
Wewe uliyetutengeneza
BWANA TUNAKUSIFU
BWANA TUNAKUSIFU EWE MUNGU

Tunaimba Haleluya
Tunaimba Haleluya
Na tunafuata nyayo zako
Kupitia kwa Yesu Mwana wa mwanadamu

***Ubeti wa pili***
Tuongoze Ewe Bwana
Kwa njia zako tujitenge na dhambi
Tukomboe kutokana na ukandamizaji
Kwa hiyo tunatii